

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



## KUKAMILIKA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI NA KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI AWAMU YA TATU

Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kukamilika kwa awamu ya pili ya uhakiki wa sifa za waombaji waliodahiliwa na Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2018/19. Majina ya waombaji waliochaguliwa katika awamu ya pili yameshapelekwa kwenye vyuo husika kwa ajili ya kutangazwa.

Tume pia imefungua dirisha la maombi awamu ya tatu kuanzia tarehe **24** hadi **26 Septemba 2018** ili kuruhusu makundi yafuatayo kuomba udahili:

- Waombaji waliokosa nafasi kwenye awamu ya kwanza na ya pili;
- Waombaji wa kidato cha sita na stahhada walioshindwa kuomba katika awamu zilizotangulia;
- Waombaji waliomaliza mitihani ya “Cambridge” mwaka 2018 na matokeo yao yameshatoka; na
- Waombaji waliokuwa wamedahiliwa miaka ya nyuma na kuacha au kukatisha masomo.

Aidha Tume inapenda kuisitiza kuwa utaratibu wa kutuma maombi ni ule ule wa kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kama ilivyokuwa katika awamu za Udahili zilizotangulia. ***Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili yari potuwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.***

Imetolewa na

**Katibu Mtendaji**  
**Tume ya Vyuu Vikuu Tanzania**  
**24/09/2018**